# Skills checklist: Reading glasses

| Mshiriki wa Mafunzo: | Mwezeshaji: | Tarehe: |
|---|---|---|

| Stadi | Maoni ya Mwezeshaji | Ndio | Hapana |
|---|---|---|---|
| **Hatua ya kwanza: Chagua** | | | |
| 1. Inaanza pale mtu aliyekidhi vigezo anapopewa miwani ya kusomea, baada ya kufanya Kipimo cha Uoni kwa mujibu wa TAP.<br>Vigezo hivyo ni:<br>• Hana Matatizo ya Afya ya Macho yaliyo dhahiri.<br>• Ana umri wa zaidi ya miaka 40<br>• Anaweza kuona umbali wa kawaida<br>• Hawezi kuona E ndogo wakati wa Kipimo cha Uoni cha TAP | | | |
| 2. Tumia Chati ya E ya miwani ya kusomea ili kuweza kuchagua lenzi stahihi zenye uwezo unaohitajika:<br>• Weka chati katika umbali unaotakiwa<br>• Mtumiaji anapaswa kufungua macho yake<br>• Angalia umbali | | | |
| 3. Kama ni ngumu kupata lenzi zenye uwezo unaohitajika basi toa rufaa kwa mgonjwa | | | |
| **Hatua ya pili: Kipimo sahihi** | | | |
| 4. Anaangalia kama miwani ina kipimo sahihi cha mhusika kwa:<br>• Upana wa miwani:<br>• Kingo ya pua na sehemu ya miwani inayosaidia pua kutokuumizwa na miwani<br>• Ngazi. | | | |
| **Hatua ya tatu: Fundisha** | | | |
| 5. Anafundisha mhusika namna ya kutumia miwani ya kusomea ikiwemo utumiaji wa mwanga unaofaa. | | | |
| 6. Anamfundisha mhusika namna ya kutunza miwani ya kusomea | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7. Anatoa taarifa ambazo mhusika anapaswa kuwa nazo ikiwemo kujua dalili za mwanzo kuhusu afya ya macho. | | | |
| **Hatua ya nne: Ufuatiliaji** | | | |
| 8. Anamuuliza mhusika kama miwani inakidhi mahitaji yake na kama haikidhi, atoe sababu ya kwanini miwani haikidhi mahitaji. | | | |
| 9. Anachukua taarifa sahihi za Ufuatiliaji | | | |
| **Kwa hatua zote** | | | |
| 10. Toa huduma salama na nzuri ambazo zinamlenga mteja zaidi wakati wote unapofuata hatua zote za matibabu | | | |

## Mambo Muhimu kwa Wawezeshaji

**Tumia Orodha ya Stadi ifuatayo kukusaidia:**

- Tathmini namna washiriki wa mafunzo wanavyotumia stadi zao kwenye kutoa miwani ya kusomea. Kujua kama:
  - Wanaweza kutoa miwani ya kusomea kwa usalama na bila kusaidiwa na mtu mwingine au
  - Wanahitaji mafunzo zaidi, na kama ndio, ni stadi gani wanahitaji kuzifanyia mafunzo?

**Kumbuka kwamba:**

- Orodha hii inaweka msisitizo kwenye stadi ambazo ni muhimu zaidi ambazo ziko kwenye moduli ya TAP
- Inawezekana kuna stadi nyingingine ambazo ungependa Washiriki wa Mafunzo kuwa nazo. Unaweza kuongeza stadi nyingine kwenye orodha hii, kama unadhani kwa kufanya hivyo itasaidia
- Unaweza usiweze kuona stadi kwenye hatua zote nne kwa kipindi cha kwanza, lakini waweza kufuatilia stadi mojawapo kwa wakati mwingine ujao.

**Kutumia Orodha ya Stadi:**

- Angalia kwa ukaribu namna Washiriki wa Mafunzo wanavyofuata hatua za utoaji wa miwani ya kusomea. Hii inawezekana kuwa kwa kufanya igizo la Mteja na Mtoa huduma ( kila mmoja aigize nafasi mojawapo) au waweza kuigiza na wateja.
- Hakikisha kuwa ufanyaji zoezi/ Igizo na mteja unafanyika kwa usalama.
- Andika kwenye fomu kama mshiriki wa mafunzo amefanya kila stadi kwa kadri inavyohitajika. Tumia eneo la kutoa maoni kutoa maelezo zaidi. Yawekana kuna mambo yaliyofanyika vizuri, au maeneo ambayo bado yanahitaji mazoezi zaidi.

**Kutoa mrejesho kwa Washiriki wa Mafunzo**

- Jadili na Washiriki wa Mafunzo kuhusu mambo uliyoyaona wakati wa Uwezeshaji. Waambie mambo wanayoyafanya vizuri, na maeneo ambao bado yanahitaji kufanyiwa mazoezi zaidi.

- Mpe Mshiriki wa Mafunzo nakala ya mambo waliyojifunza ili aweze kutunza kumbukumbu.
- Endelea kufanya uwezeshaji na kuwaacha watende wao wenye ili uweze kufanya tathmini. Fanya hivi mara kwa mara kwa kadri wanavyojifunza na stadi mpya pamoja na hali ya kujiamini.

**Je, ni wakati gani Mshiriki wa Mafunzo atakuwa tayari kugawa miwani ya kusomea bila kupata msaa wa wa Mwezeshaji?**

- Ili kutoa miwani ya kusomea kwa usalama zaidi, Mshiriki wa Mafunzo anapaswa kuendelea kujifunza ili kutekeleza stadi zote kwa usahihi
- Kumbuka- utoaji mafunzo na usimamizi ni mchakato endelevu, inayolenga kuboresha stadi.